Swali: Kwanini katika biblia lisitumike neno “Mwizi” na badala yake linatumika neno “Mwivi”…Mwivi ni nini?

---

Jibu: Mwivi na Mwizi ni Neno moja, lenye maana moja.. isipokuwa ni lugha mbili za nyakati mbili tofauti.

Kiswahili kilichotumika katika kutafsiri biblia ni Kiswahili cha zamani, kilichoitwa “kimvita” ambacho ndicho kimebeba maneno ambayo hatuyaoni katika Kiswahili cha sasa, na mojawapo ya maneno ndio kama hayo “Mwivi na wevi” ikimaanisha “mwizi na wezi”. Ndio maana katika biblia yote huwezi kukuta neno Mwizi, badala yake utakuta mwivi *(Soma Kutoka 22:2, Ayubu24:14, Zaburi 50:18, Mithali 6:30, Yoeli 2:9, Luka 12:39 n.k )*

Maneno mengine ya kimvita (Kiswahili cha zamani) ambayo mengi ya hayo hayatumiki sasa ni pamoja na “jimbi” badala ya “Jogoo”… “Kiza” badala ya “Giza”….”Nyuni” badala ya “ndege”…. “Kongwa” badala ya “Nira” na mengine mengi.

Kwahiyo kwa hitimisho ni kwamba “Mwivi” na “Mwizi” ni Neno moja, lenye maana ile ile moja (ya mtu anayeiba).

Lakini mbali na hilo, maandiko yanatufundisha kuwa Bwana YESU atakuja kama “Mwivi”..

> *Ufunuo 16:15 “(Tazama, naja kama mwivi. Heri akeshaye, na kuyatunza mavazi yake, asiende uchi hata watu wakaione aibu yake)”*

Je umewahi kujiuliza ni kwanini aje kama Mwivi na si Askari?.. Kwa upana juu ya hilo basi fungua hapa >>ANAKUJA KAMA “MWIVI” NA SI KAMA “ASKARI” FANYIKA CHOMBO CHA THAMANI.[1]

Bwana akubariki.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10[2]

Maran atha!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

KAMA MWIZI USIKU WA MANANE.[3]

Nini maana ya Mithali 6:30 Watu hawamdharau mwivi, Akiiba ili kujishibisha[4]

OKOA BADALA YA KUANGAMIZA![5]

Nini maana ya ELOHIMU?[6]

Wale waliowekewa tayari ufalme ni akina nani?. (Mathayo 20:23).[7]

Rudi nyumbani[8]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. ANAKUJA KAMA “MWIVI” NA SI KAMA “ASKARI” FANYIKA CHOMBO CHA THAMANI.:

https://wingulamashahidi.org/2021/07/15/anakuja-kama-mwivi-na-si-kama-askari-fanyika-chombo-cha-thamani/

2. https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10: https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10
3. KAMA MWIZI USIKU WA MANANE.: https://wingulamashahidi.org/2018/07/17/kama-mwizi-usiku-wa-manane/
4. Nini maana ya Mithali 6:30 Watu hawamdharau mwivi, Akiiba ili kujishibisha: https://wingulamashahidi.org/2024/01/18/mithali-630-watu-hawamdharau-mwivi-akiiba-ili-kujishibisha/
5. OKOA BADALA YA KUANGAMIZA!: https://wingulamashahidi.org/2019/05/22/okoa-badala-ya-kuangamiza/
6. Nini maana ya ELOHIMU?: https://wingulamashahidi.org/2019/08/31/nini-maana-ya-elohimu/
7. Wale waliowekewa tayari ufalme ni akina nani?. (Mathayo 20:23).: https://wingulamashahidi.org/2024/01/19/wale-waliowekewa-tayari-ufalme-ni-akina-nani-mathayo-2023/
8. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org